Kuwaokoa Wanadamu Kutoka Motoni

na

Ellis P. Forsman

Kuwaokoa Wanadamu Kutoka Motoni

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 14, 2011

Kuwaokoa Wanadamu Kutoka Motoni

Yuda 1:17-25

Yuda 1:17-25, "*Bali ninyi wapenzi yakumbukeni maneno yaliyonenwa zamani na mitume wa Bwana wetu Yesu Kristo, yakwamba waliwaambia ya kuwa, wakati wa mwisho watakuwako watu wenye kudhihaki, wakizifuata tama zao wenyewe za upotevu. Watu hao ndio waletao matengano, watu wa dunia hii tu wasio na Roho. Bali ninyi wapenzi mkijijenga juu ya imani yenu iliyotakatifu sana, na kuomba katika Roho Mtakatifu, jilindeni katika upendo wa Mungu, huku mkingojea rehema za Bwana wetu Yesu Kristo, hata mpate uzima wa milele. Wahurumieni wengine walio na shaka, na wengine waokoeni kwa kuwanyakua katika moto; na wengine wahurumieni kwa hofu, mkilichukia hata vazi lililotiwa uchafu na mwili. Yeye awezaye kuwalinda ninyi msijikwae, na kuwasimamisha mbele ya utukufu wake bila mawaa katika furaha kuuu; yeye aliye Mungu pekee, mwokozi wetu kwa Yesu Kristo Bwana wetu, utukufu una yeye, na ukuu, na uwezo, na nguvu, tangu milele, na sasa na hata milele. Amina.*"

Kwa muda mfupi nataka nikuombe kupiga picha hali inayowezekana. Inaweza kutokea.

Pengine siku moja ukirudi nyumbani kutoka kazini au safari yo yote, unajikuta kwamba umetoka nje ya barabara kwamba nyumba yako inaungua moto.

Ghafla! Unasikia sauti ya wapendwa ikitoka katika nyumba hiyo. Utafanya nini?

Nafasi ni kwamba utaingia ndani ya nyumba hiyo ili kuwaokoa wapendwa wako. Je hii si kweli? Fikiria kuhusu jambo hili! Unaweza kumtoa mtu ndani ya gari linaloungua, au nyumba, kama unaweza?

Je unaogopa moto?

Katika mazingira tofauti, watu wengi wanaogopa.

Hataivyo, kwa wakati wa dharura, watu husahau uoga wao.

Neno hili dogo (moto) unatapakaa ndani ya jumuiya, au jingo, nk., mara nyingi husababisha hofu nyingi na uoga. Watu hurukia madirishani, wakikanyaga wengine, nk., ni katika juhudi za kuukimbia moto.

Kiroho, inawezekana kwa wanadamu kuwa katika "moto."

Yuda 1:23, "*Na wengine waokoeni kwa kuwanyakua katika moto; na wengine wahurumieni kwa hofu, mkilichukia hata vazi lililotiwa uchafu na mwili.*"

Yuda anaongelea wale wanaoishi chini ya mvuto wa dhambi. Mamilioni wanasimama katika "mioto" ya hukumu.

Kama Mkristo, tuna jukumu la kuwaokoa watu kutoka motoni kabla hawajateketea.

Wanadamu wanapaswa kutubu la sivyo waangamie. Luka 13:3, "*Nawaambia sivyo, lakini msipotubu, ninyi nyote mtaangamia vivyo hivyo.*"

Kwa wakati huu tunataka kujifunza baadhi ya ukweli kuhusu kuwaokoa watu kutoka motoni. Sisi ni "waokoaji wa moto."

Kwa nini tuwaokoe wanadamu kutoka motoni

Kwa sababu tumeamuriwa kufanya hivyo

Marko 16:15-16, "*Akawaambia enendeni ulimwenguni mwote mkahubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka, asiyeamini atahukumiwa.*"

Kwa sababu ni ukaidi na hatia kutowaokoa watu kutoka motoni

Hii ni kweli katika hali ya kimwili; vipi zaidi kuhusu hali ya kiroho.

Nafsi inathamani kubwa katika dunia. Marko 8:36-38, "*Kwa kuwa itamfaidia mtu nini kuupata ulimwengu wote, akipata hasara ya nafsi yake? Ama mtu atoe nini badala ya nafsi yake? Maana kila mtu atakayenionea haya mimi na maneno yangu katika kizazi hiki cha uzinzi na dhambi, Mwana wa Adamu atamwonea haya mtu huyo, atakapokuja katika utukufu wa Baba yake pamoja na malaika watakatifu.*"

Unaweza kuokoa kijiti kutoka motoni. Vipi kuhusu mwanadamu?

Kwa sababu ya mauaji ya moto

Huenda haraka na inapaswa kushughulikiwa kwa haraka. Haijui mipaka au ukomo.

Lazima tujaribu kuwaokoa wengine wasife katika dhambi zao.

Yoh. 8:21-24, "*Basi akawaambia tena, mimi naondoka nanyi mtanitafuta; nanyi mtakufa katika dhambi yenu; nami niendako ninyi hamwezi kuja. Basi Wayahudi wakasema, je! Atajiua! Kwa kuwa asema mimi niendako ninyi hamwezi kuja? Akawaambia ninyi ni wa chini, mimi*

ni wa juu; ninyi ni wa ulimwengu huu, mimi si wa ulimwengu huu. Kwa hiyo naliwaambieni mtakufa katika dhambi zenu; kwa sababu msiposadiki ya kuwa mimi ndiye, mtakufa katika dhambi zenu."

Kwa sababu tukishindwa, ni nani atakayeweza?

Mungu hajawaagiza malaika kufanya hii kazi.

Ibilisi hawezi kuifanya.

Wasiomjua Mungu, wasiomcha hawawezi kuifanya.

Lazima tuifanye! Tunaokolewa ili kuwaokoa wengine.

Kwa sababu tusipoifanya sasa, baada ya kufa, itakuwa imechelewa.

Kwa nini wanadamu hawapendi kuokolewa kutoka motoni

Hii haiwezi kufikiriwa katika hali ya kimwili. Mwanadamu ye yote angependa atoke motoni. Muda mwingi umeendelea kwa wanadamu kuukimbia moto.

Katika hali ya kiroho, baadhi ya watu hawajui kwamba wako katika "moto"

Kiberiti hupigwa; tochi huwashwa.

Hawaangalii matendo yao kuwa mabaya, kwa sababu wanatazama kupitia macho yao, na sio ya Mungu.

Hata wale waliorudi nyuma wasioenda kanisani wanakataa.

2 Pet. 2:20, "*Kwa maana wale waliokwisha kuyakimbia machafu ya dunia kwa kumjua Bwana na Mwokozi Yesu Kristo, kama wakinaswa tena na kushindwa, hali yao ya mwisho imekuwa mbaya kuliko ile ya kwanza.*"

Wengine wameukataa ukweli kuhusu hukumu

Wanasema "jehanamu" iko hapa katika maisha haya.

Wengi hawaamini katika mfumo wo wote wa jehanamu.

Wengine wanadhania kuwa wanaweza kutoka motoni wao wenyewe

Wanashindwa kujua kwamba nguvu iko katika injili, na si katika mwanadamu.

Rum. 1:16, "*Kwa maana siionei haya injili; kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu, kwa kila aaminiye, kwa Myahudi kwanza na kwa Myunani pia.*"

Mwanadamu hawezi kujiokoa mwenyewe. Rum. 10:13-17, "*Kwa kuwa kila atakayeliitia jina la Bwana ataokoka. Basi wamwiteje yeye wasiyemwamini? Tena wamwaminije yeye wasiyemsikia? Tena wamsikieje pasipo mhubiri? Tena wahubirije wasipopelekwa? Kama ilivyoandikwa, ni mizuri kama nini miguu yao wahubirio habari ya mema! Lakini si wote walioitii ile habari njema. Kwa maana Isaya asema, Bwana ni nani aliyeziamini habari zetu? Basi imani chanzo chake ni kusikia na kusikia huja kwa neno la Kristo.*"

Wengine wanadhani kwamba wanamuda mwingi

Watatoka nje kama wakiwa tayari.

Ukengeufu unaua. Kesho inaweza kuchelewa sana.

Kutingwa

Shetani. Yoh. 8:44, "*Ninyi ni wa baba yenu ibilisi, na tama za baba yenu ndizo mpendazo kuzitenda. Yeye alikuwa mwuaji tangu mwanzo; wala hakusimama katika kweli, kwa kuwa hamna hiyo kweli ndani yeke. Asemapo uongo husema yaliyo yake mwenyewe; kwa sababu yeye ni mwongo na baba wa uongo.*"

Mwanadamu.

Nilipokuwa na mika 20, ghala la jirani yangu liliwaka moto. Kulikuwa na baadhi yetu waliokuwa wakijaribu kuokoa vyombo vyake kutoka ghalani. Moto uliwavutia wengi walikuja kujionea, lakini walikuwa wanaingia njiani. Waliegesjsha magari yao pembeni mwa barabara nyembamba ili kwamba magari ya zima moto yasiweze kufika na kuuzima moto. Mmoja wa watu waliotusaidia kuuzima alikuwa ni mwandishi wa gazeti. Aliandika mlolongo wa moto kwenye gazeti siku iliyofuata. Aliwashutumu waliozuia jitihada za uokoaji na kuuzima moto.

Kuna wale wanaozuia mwendelezo wa wale wanaomtumikia Kristo katika kujaribu kuwaokoa wengine na moto wa milele.

Mat. 24:24, "*Kwa maana watatokea makristo ya uongo, na manabii wa uongo, nao watatoa ishara kubwa na maajabu; wapate kuwapoteza, kama yamkini hata walio wateule.*"

Jinsi ya kuwaokoa wanadamu kutoka motoni

Kwa upendo na huruma katika moyo wa mtu na kwa shauku kubwa

Leo ndio siku.

Nafsi huteketezwa kila sekunde.

Kwa umakini

Jiangalie mwenyewe. Gal. 6:1-2, "*Ngugu zangu mtu akighafilika katika kosa lolote ninyi mlio wa Roho mrejezeni upya mtu kama huyo kwa roho ya upole, ukijiangalia nafsi yako usije ukajaribiwa wewe mwenyewe. Mchukuliane mizigo na kuitimiza hivyo sheria ya Kristo.*"

Huu ni ukuu "kazi ya uokoaji" katika ulimwengu.

Kwa kutumia "vifaa" sahihi na "vyombo"

Neno la Mungu.

- Yoh. 8:32, "*Tena mtaifahamu kweli nayo hiyo kweli itawaweka huru.*"
- Efe. 6:11, "*Vaeni silaha zote za Mungu mpate kuweza kuzipinga hila za shetani.*"

Kwa kutoingia "katika" "moto" wewe mwenyewe

Lazima uwe na taadhari katika kuwaokoa wanadamu kutoka motoni. Usiungue!

Usishindwe na dunia.

Tunapaswa kujifunza sisi wenyewe namna ya kuwaokoa watu kutoka motoni. Ukitambua mitego ya shetani na silaha za moto.

Kwa ujasiri mkubwa na nguvu

Kumbuka Mungu anafanya kazi pamoja na wewe. Unaweza kuwa mshindi katika Kristo.

Waoga watakuwa katika ziwa la moto.

Ufu. 21:8, "*Bali waoga, na wasioamini, na wachukizao, na wauaji, na wazinzi, na wachawi na hao waabuduo sanamu, na waongo wote sehemu yao ni katika lile ziwa liwakalo moto na kiberiti. Hii ndiyo mauti ya pili.*"

Hitimisho

Je uko “motoni”?

Je unataka kuokolewa kutoka motoni? Huwezi kutoka kwa nguvu zako.

Yesu alikuja kukuokoa kutoka katika moto, na kukusaidia kuiepuka milele. Unaweza, kwa imani kushikilia mapenzi yake, injili, na kuitii?

Kama muumini wa kanisa aliyerudi nyuma, unatakiwa kutubu na kuokolewa kutoka motoni, pia.

Usiwapeleke wengine motoni pamoja na wewe.

Je, unamajukumu ya kuwaokoa wengine kutoka “motoni”?

Utapotea kama hutafanya jaribio.

Mungu na atusaide kwa haraka kutoka katika “mwali wa dunia,” na tuwaokoe wanadamu wanaoangamia.